# OFISI YA RAISI
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**Ofisi ya Mkuu wa Shule,**

**P. O. BOX 2276,**

**DAR ES SALAAM.**

Telephone: +255 762828626 Email: jangwanisecondaryschool@gmail.com

Jina la Mwanafunzi ……………………………………………………………...

S.L.P …………………………………………………………………………...

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA JANGWANI KIDATO CHA KWANZA 2025**

### 1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari kidato cha kwanza mwaka 2025

Shule ya sekondari Jangwani ipo mkoa wa Dar es salaam, Manispaa ya Jiji la Dar es Salaam, Tarafa ya Kariakoo, kata ya Upanga Magharibi, umbali wa kilometa tatu kutoka katikati ya mji.

Usafiri wa basi unapatikana kwa urahisi kwa vile shule ipo kwenye barabara inayoelekea Hospitali kubwa ya Muhimbili, kituo cha fire (faya).

### 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

#### A. SARE ZA SHULE

i. Wanafunzi wasiovaa hijabu

Sketi mbili za rangi ya karoti inchi tano chini ya goti na mashati mawili meupe ya mikono mifupi.

ii. Wanafunzi wanaovaa hijabu

Sketi mbili ndefu za rangi ya karoti zinazofunika vifundo vya mguu na mashati mawili ya mikono mirefu yanayofunika makalio.[isiwe nusu kanzu]

**ANGALIZO;**

i) Sare hizi zisiwe zinabana mwili.
ii) Juba lifunike vifundo vya mikono na livuke nyonga, **kitambaa cha halua cheupe kitumike**.

#### B. SARE ZA MICHEZO
Sare za michezo kwa shule hii ni T-Shirt ya rangi ya kijivu (1) na Bukta sketi ya rangi ya karoti (angalia kiambatanisho)

#### C. SARE YA SWETA
Sare ya sweta la shule kwa wale wanaohitaji linapatikana shuleni.

**D. VIATU VYA SHULE**

i. Viatu vya shule ni raba nyeupe zenye gidamu (Kamba) zisizo na maandishi wala alama yeyote. Pia zisiwe na soli nene.

ii. Soksi nyeupe zisizo na alama wala maandishi, na zisivuke goti. Zingatia michoro kwenye ukurasa wa 5.

E. Mwanafunzi awe na nywele fupi zinazochanika kwa kitana kidogo.

### 2.1 VIFAA VYA DARASANI (SHAJARA)

a) Madaftari makubwa 10 (**Quire 3**)
b) Kalamu za kuandikia, mkebe wa hesabu (mathematical set), rula ndefu, penseli na mfutio.
c) Vitabu vya sekondari kidato cha kwanza (TIE), atlas na kamusi ya kiingereza kwa kiingereza (dictionary)
d) Madaftari madogo 10 (msomi yenye kurasa 80) kwa ajili ya mazoezi.
e) Flat file kwa ajili ya kutunzia taarifa za mwanafunzi na ripoti zake za taaluma.
f) Vitabu viwili vya Kiingereza kati ya vifuatavyo:- Mabala the Farmer, Hawa the Bus Driver na The Magic Garden.

### 2.2 CHAKULA

Shule haitoi chakula kwa mwanafunzi wa kutwa, aje na fedha kwa ajili ya kununua chakula.

### 2.3 NAULI

Shule haina usafiri, kila mwanafunzi wa kutwa anajitegemea kwa usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani, hivyo awe na nauli ya kutosha.

2.4 Mahitaji mengine kulingana na mahitaji yake binafsi.

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya ellimu na .25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Raisi- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji wa Ellimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shule.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii yote kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation/Remedial)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Jutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kkuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa. Unapokuwa eneo la shule na nje ya eneo la shule kwa shughuli za kishule.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali za umma.
j) Huruhusiwi kupaka hina, wanja, lip stick, rangi za kucha, kunyoa nyusi, wala urembo wowote.
k) Ni marufuku kuwa na simu ya mkononi shuleni. Endapppo kuna jambo lolote la dharura simu ya shule itatumika.

**1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**


a) Wizi
b) Uasherati au Ushoga

c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama viel uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya taifa
h) Kkuwa mjamzito/mimba
i) Kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu.
m) Kuwa na simu ya mkononi
n) Kutokuwa na sare ya shule ukiwa katika mazingira ya shule.
o) Kutokuhudhuria masomo kwa Zaidi ya siku tisini bila taarifa.
p) Kutumia lugha ya matusi.

**F. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

A. Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
B. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutokushiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai.
C. Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
D. Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu watakaotambulika kuhusika na mwanafunzi.
E. Picha tatu za mwanafunzi.

5. Ifuatayo ni michoro yenye kuonyesha namna sare inapaswa kuonekana baada ya kushonwa



# FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA

PICHA YA MWANAFUNZI

**Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi: -**

1. Majina kamili ya mwanafunzi: [Matatu] ………………………………………………
2.Uraia: -………………………………………………………………………………
3.Dini: - ……………………………………………………………………………...
4. Tarehe ya kuzaliwa na Namba ya cheti cha kuzaliwa:- ………………………………
5. Mkoa/Wilaya asili ya mwanafunzi: - ……………………………………………….

6. Sio yatima/Yatima/ Mzazi mmoja, Kama mzazi mmoja ni baba tu/ mama tu [**Kata isiyohusika**]
7. Shule uliyosoma kabla ya kuja Sekondari ya Jangwani

| **MAJINA MATATU YALIYOANDIKISHWA SHULENI** | **SHULE YA MSINGI ULIKOSOMA** | **MWAKA ULIOANZIA** | **MWAKA ULIOTOKA** |
|---|---|---|---|
| | | | |

KAMA MUHAMIAJI TAARIFA ZA UHAMIAJI

| SHULE ULIYOTOKA | WILAYA | MKOA | KIDATO | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

Prem No. yako ni ……………………………………….

Mawasiliano ya Mkuu wa Shule ulikotoka …………………………………............

Sahihi ya mwanafunzi …………………………. Tarehe ……………………………

PICHA YA MZAZI/MLEZI

**Sehemu hii ijazwe na Mzazi/ Mlezi:-**

1. Jina kamili la mzazi/ mlezi:- ……………………………………………………………
2. Uraia ………………………. Namba ya cheti cha uraia …………………………………
3. Anuani kamili ya makazi [ Mtaa, Kata, Wilaya ] …………………………………………

   ……………………………………………………………………………………..

4. Namba ya simu ya baba/ mlezi …………………………………………………………
5. Namba ya simu ya mama/ mlezi ……………………………………………………..

PICHA YA NDUGU MWINGINE

6. Kazi anayofanya mzazi/ mlezi ( kama vile Daktari, mwalimu, fundi n.k) ……………………....................

**Ndugu wengine wa karibu :-**

| | Jina la ndugu | Anapoishi | Uhusiano | Namba ya simu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |

Sahihi ya mzazi/ mlezi ……………………………….. Tarehe …………………………..

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ……………………………………………………………………………… ( Majina matatu )

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote na nimekubali kujiunga na shule ya Sekondari ya Jangwani kuanzia tarehe ………………………………….

2. Naahidi kwamba :-

a) Niitazingatia sheria zote za shule na kutimiza wajibu wangu kama mwanafunzi.

b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo vilivyo kinyume na sheria za shule na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c) Nitatunza mali ya Umma ambayo ni pamoja na Majengo, Samani, Vitabu , vifaa vya maabara na vifaa vinginevyo nitakavyokabidhiwa.

d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yeyote stahiki endapo nitakiuka maelekezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

Saini ya mwanafunzi: ………………………………. Tarehe: ……………………………

## AHADI YA MZAZI/ MLEZI

Mimi …………………………………………………. Ni Mzazi/ Mlezi wa ……………………………………

wa kidato cha ………… mwaka ………………... naahidi kwamba: -

1. Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni kuhakikisha kuwa atazitii sheria zote za shule na kuyazingatia mambo yote yaliyotajwa.
2. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shuleni kila siku saa kabla ya saa 1:00 asubuhi.
3. Nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kuhakikisha mwanafunzi anahitimu kidato cha nne/ sita. Yaani anasoma hadi anamaliza kadiri inavyotakiwa.
4. Ninaruhusu mwanangu achukuliwe hatua yeyote stahiki endapo atavunja mojawapo ya sheria na kanuni zilizoorodheshwa.

Saini ya Mzazi/ Mlezi ………………………………… Tarehe …………………………….

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**ILALA MUNICIPAL COUNCIL**

Head of School's Office,

P. O. BOX 2276,

DAR ES SALAAM.

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A.

To the medical officer

______________________________________________

Miss __________________________________________

Please examine the above named student for her full time secondary school studies.

Date _____________________________ Signature __________________________

Headmistress.

PART B.

MEDICAL CERTIFICATE

(**To be completed by a medical Officer at a Healthy Centre level and above**)

Put a tick (√) for positive and a cross (×) for negative in a box provided.

| | |
|---|---|
| Pregnancy | |
| Asthma | |
| Sight | |
| Diabetes | |
| Worms (Stool Test) | |
| Epilepsy | |
| T.B (Tuberculosis) | |
| Sickle Cell | |
| Heart Disease | |
| Yellow Fever | |
| U.T.I | |
| Venereal Diseases | |
| Leprosy | |
| Other Problems and Physical Impairment | |

I have examined the above named student and concluded that she is physically fit for full time secondary school studies.

Date ___________________ Signature _____________________

Station ____________________ Designation ___________________ Official Stamp